

**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS(TAMISEMI)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO**

SHULE YA SEKONDARI UBIRI  
S.L.P 308,  
LUSHOTO.

---

Kumb.Na:UBSS/JI/ADV/V.1/2018/1

-----,  
-----,

**YAH:KUCHAGULIWA KIDATO CHA 5 MWAKA 2018/2019 UBIRI SEKONDARI**

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha tano mwaka 2018 katika shule ya Sekondari ya **UBIRI** iliyoko Lushoto mjini katika mkoa wa Tanga. Ufikapo Lushoto mjini utapanda magari yanayoelekea Soni – Mombo, na kwa wanaotoka Mombo – Soni shuka kituo kinachojulikana kama **MALWATI** na hapo utaona kibao kinachoelekeza shule ilipo.

Umechaguliwa kutokana na ufaulu mzuri wa mitihani yako ya kidato cha nne mwaka 2017. Hivyo,ukiwa Ubiri unatakiwa kusoma kwa bidii na maarifa, ili uitumie nafasi uliyopewa na jamii na Serikali vizuri kwa manufaa yako binafsi, jamii na serikali.

UkiwaUbiri Sekondari utalazimika kufuata **Sheria,Taratibu,Kanuni na Maadili ya uanafunzi**(Sheria za Shule zimeambatanishwa).Ukienda kinyume na Sheria hizi utafukuzwa shule, kwani **utovu wa nidhamu hautavumiliwa**.

Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..... kabla ya saa kumi Jioni, bila kukosa tayari kwa kuanza masomo tarehe .....

Utajaza kiambatanisho **A na B**-Fomu ya kujua afya(Medical Examination Form) na ufike navyo shuleni siku ya kuripoti.

Ufike na nakala halisi ya cheti cha kuzaliwa na resultslip pamoja na nakala zake. Kama huna, nenda Mahakamani ili **Uape upewe Affidavit**, kuthibitisha kuwa wewe ni raia wa Tanzania.

**MAHITAJI MUHIMU YA SHULE**

**1. Sare ya Shule**

- (a) Mashati 2 meupe ya Mikono Mifupi,Tetrone(Lisiwe linalo bana au linalo oneshwa ndani)
- (b) Masweta 2 ya rangi ya Bluu iliyokolea ( dark blue) ya 'V' (yasiwe ya vifungo)
- (c) Sketi 2 zinazovuka magoti za heshima za rangi Bluu iliyokolea (Dark Blue) mshono uwe ''rinda box''katikati na marinda matatu kila upande yaani kulia na kushoto.
- (d) Viatu vyeusi vya ngozi jozi 2 vya kufunga na kamba(visiwe vyenye visigino virefu), na soksi nyeupe.
- (e) Tai mbili za kipepeo za rangi ya bluu iliyokolea (dark Blue) kwa wale wasiovaa Hijab
- (f) Shuka 2 za rangi ya pink
- (g) Blanketi, au mashuka mazito ya kujifunika.
- (h) Picha nne passport size

- (i) Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa isipokuwa masweta kwa ajili ya kujikinga na baridi
  - (j) Godoro imara la ukubwa wa futi mbili na nusu kwa sita.(Godoro Dodoma au Comfy)
  - (k) Magauni mawili ya rangi ya kijivu (Grey) yawe ya kitambaa kizito kisichoonyesha nguo za ndani mshono uwe rinda Box.
  - (l) Kwa wanafunzi wa kiislamu watakaopenda kuvaa Hijabu wataruhusiwa kavaa sketi ndevu za dark blue, mashati meupe (nusu kanzu), sweta la dark blue na Hijabu nyeupe tu isiyo na urembo.
  - (m) Sanduku la bati (Tranker)
  - (n) Track suit ya rangi ya kijani na raba kwa ajili ya michezo
- NB: wanafunzi wote hawaruhusiwi kusuka/ ama kufuga nywele**

## **2. Zana za Kazi na Usafi**

- (a) Ufike na daftari za kutosha kwa masomo 4 utakayo soma,kalamu na mkebe(Mathematical Set kwa watakaosoma somo la Jiografia)
- (b) Karatasi kwa ajili ya mitihani Rimu 1-A4
- (c) Dictionary ya kiingereza kwa kiingereza 1, kamusi ya kiswahili kwa kiswahili Ina kiswahili kwa kiingereza 1 kwa matumizi binafsi na kwa masomo ya tafsiri na ukalimani kwa somo la Kiswahili na Kiingereza.
- (d) Ufike na sahani, kikombe, kijiko na ndoo ndogo moja na kubwa moja.
- (e) Kwa wanafunzi wa HGL waje na jembe lenye mpini na kwanja na kwa HKL waje na jembe lenye mpini na reki.

## **3. Ada na Michango mbalimbali ya shule**

- (a) Ada ya shule ni sh.70,000/=kwa mwaka,unaruhusiwa kulipa sh.35,000/= kwa muhula
- (b) Taaluma ni sh.20,000/= kwa mwaka inalipwa mara moja kila mwanzo wa mwaka wa masomo.
- (c) Mchango wa mahafali Tshs 10,000/= kwa mwaka
- (d) Kitambulisho sh.6,000/=
- (e) Mitihani ya kujipima (mock) sh. 20,000/=
- (f) Tahadhari sh.5,000/=(Ambayo hairudishwi)
- (g) Sh.15,000/= tu za mchango ujenzi/ukarabati.
- (h) Nembo ya shule 2,000/=
- (i) Huduma ya kwanza/ afya kwa mwaka sh. 10,000/=
- (j) T-shirt za shule moja sh. 10,000/=
- (k) Walinzi, wapishi na vibarua wengine sh. 30,000/=

**JUMLA YA ADA NA MICHANGO NI TSH. 198,000/=**

**N:B 1. Ada na michango yote italipiwa benki kwenye akaunti ya Shule ya Sekondari UBIRI namba 4163500079 NMB BRANCH.**

**2. Mwanafunzi atapokelewa tu iwapo amekamilisha kulipa ada,michango mingine na kukabidhi vifaa vyote vilivyoagizwa akiwa na risiti ya malipo ya benki (BPS). Hivyo mwanafunzi ambaye hatofika na vifaa na michango iliyoagizwa hatapokelewa.**

Tunashauri mwanafunzi awe na fedha za mfukoni (pocket money).

Unaposafiri,**uvae sare ya shule na ufike shuleni ukiwa katika sare ya shule.**Utakapofika shuleni ripoti kwenye ofisi ya Mkuu wa Shule ili upokelewe rasmi.

***HAKIKISHA UNASOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.***

Karibu sana Shule ya Sekondari Ubiri.

.....

**SELESTINA L.IFANDA**

**Mkuu wa Shule (0764 260 023/ 0788 340 031)**

**Makamu mkuu wa shule (0718 723 776)**